**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA KAMATI YA BAJETI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA KUTOZA KODI NA KUREKEBISHA BAADHI YA SHERIA ZA FEDHA NA KODI KUHUSIANA NA UKUSANYAJI NA UDHIBITI WA MAPATO YA SERIKALI KWA MWAKA 2021/2022

## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu (SW), mwingi wa rehema mwenye kurehemu kwa kuendelea kutukarimu neema zake zisizo na kifani. Tunamuomba atuzidishie hekima na busara katika kutimiza wajibu wetu wa kujadili, kushauri na hatimae kuupitisha Mswada huu wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kurekebisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali kwa mwaka 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kukushukuru wewe binafsi, pamoja na wasaidizi wako Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Baraza kwa uongozi wenu mahiri katika kipindi chote tokea kuanza kwa Baraza hili la Kumi (10). Aidha, nikushukuru pia kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu, ili kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kurekebisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali kwa mwaka 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,** Hotuba hii isingeweza kukamilika bila ya mashirikiano makubwa waliyonipatia Wajumbe wenzangu wa Kamati na zaidi Mwenyekiti wetu Mhe. Ali Suleiman Ameir katika kuupitia Mswada huu. Hivyo, kwa dhati kabisa napenda kuwapongeza Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Bajeti kwa ushirikiano wao ambao umepelekea zoezi la kupitia Mswada huu kukamilika kwa ufanisi mkubwa. Kwa ruhusa yako, naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo;-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Ali Suleiman Ameir | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Anna Athanas Paul | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Harusi Said Suleiman | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Issa Haji Ussi Gavu | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Miraji Khamis Mussa | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Prof. Omar Fakih Hamad | Mjumbe |

Aidha, napenda kuishukuru kwa dhati kabisa Sekreteriati ya Kamati ya Bajeti inayoundwa na makatibu wanne na msaidizi wa mjumbe, naomba pia niwatambue kwa majina yao kama ifuatavyo;

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Abdalla Ali Shauri | Katibu |
| 2. | Ndg. Asha Said Mohamed | Katibu |
| 3. | Ndg. Shaib Fadhil Shaib | Katibu |
| 4. | Ndg. Yussuf Mkamba Mwinyi | Katibu |
| 5. | Ndg. Yustina E. Joseph | Msaidizi wa Mjumbe |

## UCHAMBUZI WA MSWADA

**Mheshimiwa Spika,** Madhumuni ya Mswada huu ni kurekebisha Sheria mbali mbali za Fedha na Kodi zinazohusika na ukusanyaji na usimamzi wa Mapato ya Serikali na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kufikia matarajio ya ukusanyaji wa mapato kwa mfumo wa ulipaji kodi na kuweka mazingira wezeshi ya biashara nchini, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imekusudia kuchuka hatua kadhaa za kurekebisha Sheria mbali mbali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu iliupitia Mswada huu na kuibua marekebisho mbali mbali, baadhi ya marekebisho hayo ni pamoja na marekebisho ya kisarufi ambapo vifungu mbali mbali vimerekebishwa ili kuvifanya visomeke vizuri na vilete maana iliyokusudiwa, marekebisho mengine yaliyopendekezwa na Kamati yangu ni kufanya marekebisho yanayotokana na makosa ya kiuchapaji kwa lengo la kuweka bayana usahihi wa maneno hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa Sheria zinazorekebishwa ni Sheria ya Ushuru wa Hoteli Nam.1 ya 1995 ambayo inarekebishwa kwa kuingizwa Kifungu kidogo kipya cha 3(1)(a)-(b) ambacho kina lengo la kuziba mianya ya baadhi ya wafanyabiashara wanaokwepa kulipa kodi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaafikiana na marekebisho hayo kwasababu yataondoa malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara waliosajiliwa chini ya Sheria ya Ushuru wa Hoteli juu ya wananchi ambao hugeuza nyumba za makaazi na kuwa za kibiashara bila ya

kuzingatia utaratibu wa biashara ya hoteli. Hatua hii pia itasaidia kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwengine, katika Sheria ya Rufaa za Kodi Zanzibar Nam. 1 ya 2006, Kamati inapendekeza kuondoshwa kabisa Kifungu kidogo kipya cha 3 kinachompa Waziri uwezo wa kuandaa kanuni za utatuzi wa migogoro ya kikodi. Kwa vile msingi wa kifungu hichi ni kumpa nguvu Waziri (Power of the Minister) lakini kimewekwa sehemu ya nguvu ya bodi (Power of the Board), jambo ambalo si sahihi. Kamati inashauri, kuondoshwa kifungu hichi na badala yake utaratibu wa njia mbadala za kutatua migogoro ya kodi uwe ni kutengenezwa sheria ndogo ndogo (rules).

**Mheshimiwa Spika,** Katika Sheria ya Makampuni Nam.15 ya 2013, katika marekebisho ya Kifungu cha 238, Kamati imependekeza kuingizwa maneno **"endapo itafungua biashara Zanzibar"** badala ya **"endapo imeanzisha eneo la biashara Zanzibar".** Sababu ya marekebisho hayo ni kuziwezesha kampuni kutoka Tanzania Bara kuchangia katika uchumi wa Zanzibar kwa kulipa Kodi ya Mapato Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria nyengine iliyorekebishwa katika Mswada huu ni Sheria ya Ongezeko la Thamani Nam. 4 ya 1998 ambapo Serikali inakusudia kufuta Kodi ya VAT wakati wa kuingiza bidhaa Zanzibar kutoka Tanzania Bara. Kamati inaipongeza sana Serikali kwa uamuzi huu ambao unatarajiwa kuondosha kero ya siku nyingi ya

wafanyabiashara wa Zanzibar kulipa kodi mara mbili wakati wanapoingiza bidhaa kutoka Tanzania Bara. Hata hivyo, Kamati inaisisitiza Serikali kusimamia vyema jambo hili ili kuhakikisha marekebisho haya yanatekelezwa kwa vitendo na hatimae kuwanufaisha walengwa.

**Mheshimiwa Spika,** Katika marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Nam. 12 ya 2016 pamoja na mambo mengine, Serikali inakusudia kuanza kukusanya fedha zote za umma kupitia mfumo mpya wa kielektroniki ujulikanao kama "ZanMalipo". Kamati inapata faraja sana kusikia jambo hili, ambalo bila ya shaka litasaidia sana katika kudhibiti uvujaji wa mapato ya Serikali sambamba na kupunguza gharama za ukusanyaji. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa jambo hili linaanza kutekelezwa kwa haraka. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati madhubuti itakayokabiliana na changamoto za mitandao ili jambo hili liweze kutekelezwa bila ya vikwazo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwengine, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanya marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mapato Nam. 7 ya 1996 kwa kumpa Mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kimsingi kifungu hichi kinaondoa utata wa Sheria hiyo kupingana na Katiba ya Zanzibar ambayo imempa mamlaka Mdhibiti kukagua taasisi za Serikali wakati Sheria hiyo ilikuwa imempa uwezo Waziri kuchagua mkaguzi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa marekebisho ya Sheria ya Ada ya Huduma za Bandari Nam. 2 ya 1999 kwa kumpa uwezo Kamishna kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa kuondoa urasimu na muhali katika ukusanyaji wa tozo za bandari kwa kuteuwa na kufuta uteuzi wa mawakala wa tozo anapohisi hakuna ufanisi katika ukusanyaji wa tozo hizo, jambo ambalo litaongeza mapato ya bandari na nchi kwa ujumla. Hata hivyo, Kamati inaomba jambo hili liwekewe utaratibu mzuri katika kanuni ili kuepusha Kamishna kutumia vibaya madaraka yake.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa ufafanuzi wa kina wa baadhi ya marekebisho yaliyopendekezwa na Kamati ya Bajeti, nawaomba Wajumbe wako waupitie waraka wa Kamati wa Mapendekezo ya Marekebisho ya Mswada huu ambao wamepatiwa.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kumalizia napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Mswada huu. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wote kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa. Kwa kuwa Hotuba hii ndio ya mwisho, kwa niaba ya Kamati, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza pamoja na Wajumbe wote wa Baraza kwa ushiriakiano wao walioipatia Kamati ya Bajeti. Aidha, naomba pia kuwashukuru Mawaziri pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano na kwa kuipatia taarifa mbali mbali

zilizohitajika pamoja na kufika mbele ya Kamati hii kila walipoombwa kufika.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati ya Bajeti, natoa shukrani za dhati na za kipekee kwa ***Mheshimiwa Dkt. Saada Mkuya Salum*** na ***Mhe. Miraji Khamis Mussa*** ambao walipata fursa ya kuiongoza Kamati ya Bajeti katika vipindi tofauti. Ushauri na miongozo yao, ilijenga msingi imara na kuifanya Kamati yetu iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kamati ya Bajeti tunasema asanteni sana tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu (S.W) awafanyie wepesi katika kufanikisha majukumu yenu ya sasa.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya shukran hizo maalum na mahsusi, sasa nawaomba Wajumbe wa Baraza lako, wauchangie, waujadili, na hatimae kuupitisha Mswada huu, kwa lengo la kukuza ufanisi na udhibiti wa mapato ambao utapelekea kuongezeka kwa mapato ya nchi yetu kwa taasisi zilizopewa jukumu la kukusanya mapato**.**

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwasilisha.

Ahsante,

Mhe. Ali Suleiman Ameir,
Mwenyekiti,
Kamati ya Bajeti,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**